



Muhamed Said Kiluwa

MWEKEZAJI MBARONI KWA KUMPA HONGO WAZIRI

Na Mussa Misalaba

Dar es Salaam

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imemtia mbaroni mwekezaji wa kiwanda cha Kiluwa Steel kilichopo Kiluvya wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Muhamed Said Kiluwa , kwa tuhuma za kumpa hongo Waziri wa Aridhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi.

Mtuhumiwa ambaye pia ni mfanyabiashara na mbia katika kiwanda cha Kiluwa Steel alikamatwa na TAKUKURU Julai 16, 2018 kwenye ofisi za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zilizopo Dar es Salaam.

Mtuhumiwa alimpa waziri Dola za Marekani 40, 000 ili amsaidie kupata hati 20 za ardhi kwa kuwa zile 50 alizokuwa amepewa awali na wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi zilikuwa hazimtoshi katika uwekezaji wake.

Mtuhumiwa alitenda kosa hili kinyume na kifungu cha 15(1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007 na atafikishwa mahakamani uchunguzi utakapokamilika.